

**MKATABA WA HUDUMA YA UFUNDI WA UKARABATI WA JENGO LA MASHINE
YA UPIMAJI WA VIUNGO VYA NDANI YA MWILI WA BINADAMU (ULTRAL
SOUND) NA KIPIMO CHA KUANGALIA MOYO (ECG)**

KATI YA

**MGANGA MFAWIDHI
(MWAJIRI)**

NA

**NOAH NDOMBA EDSON
(MWAJIRIWA)**

**MKATABA WA HUDUMA YA UFUNDI WA UKARABATI WA JENGO LA MASHINE
YA UPIMAJI WA VIUNGO VYA NDANI YA MWILI WA BINADAMU (ULTRAL
SOUND) NA KIPIMO CHA KUANGALIA MOYO (ECG)**

KATI YA

MGANGA MFAWIDHI sanduku la posta 5, Songea (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mwajiri) kwa upande mmoja.

NA

NOAH NDOMBA EDSON mwenye namba za simu 0784412817 (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mwajiriwa kwa upande mwingine)

KWAKUWA Mwajiri anahitaji na yuko tayari kumwajiri mwajiriwa kwa ajili ya kutoa Huduma ya ufundi wa ukarabati wa jengo la mashine ya upimaji wa viungo vya ndani ya mwili wa binadamu (ultral sound) na kipimo cha kuangalia moyo (ECG)

NA KWAKUWA Mwajiriwa yuko tayari kutoa Huduma ya ufundi wa ukarabati wa jengo la mashine ya upimaji wa viungo vya ndani ya mwili wa binadamu (ultral sound) na kipimo cha kuangalia moyo (ECG) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kupitia **Mkataba Na. ME/007/2021/2022/SORRH/W/01** kwa gharama ya Tsh **3,705,000** Kwa muda wa Mwezi mmoja (1)

HIVYO BASI pande zote mbili zinashuhudia makubaliano yafuatayo:-

1. **KWAMBA** Mkataba huu niwa muda wa mwezi mmoja kuanzia tarehe 10/01/2022 mpaka tarehe 10/02/2022.
2. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kutoa vifaa vya Ujenzi vya kiwandani na visivyo vya kiwandani vitakavyo ainishwa na kamati ya Ujenzi.
3. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kutunza vifaa vilivyo nunuliwa.
4. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kumlipa mwajiriwa gharama ya Tsh **3,705,000** (Milioni Tatu Laki saba na Elfu tano tu)
5. **KWAMBA** Malipo ya kipengele namba nne (4) yatafanywa kulingana na kazi iliyo fanyika na kisibitishwa na Kamati ya Ujenzi.
6. **KWAMBA** Hakutakuwa na mabadiliko ya aina yoyote katika kipindi chote cha Mkataba.

7. **KWAMBA** Mwajiriwa atakuwa na wajibu wa kutoa Huduma ya ufundi wa ukarabati wa jengo la mashine ya upimaji wa viungo vya ndani ya mwili wa binadamu (ultral sound) na kipimo cha kuangalia moyo (ECG) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea.
8. **KWAMBA** Mwajiriwa anapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu kutoka kwa Mhandisi wa Ujenzi.
9. **KWAMBA** Mwajiriwa anatakiwa kutunza siri za Mwajiri atakazo zijua katika kipindi chote cha Mkataba huu.
10. **KWAMBA** Mwajiriwa anatakiwa kuhakikisha kuwa eneo la Ujenzi ni safi mda wote.
11. **KWAMBA** Mwajiriwa atakuwa na wajibu wa kufanya kazi kwa uaminifu na pasipo kumsababishia hasara yoyote mwajiri
12. **KWAMBA** Mwajiriwa anatakiwa kutumia sehemu ya malipo yake kwa ajili ya kuwalipa wasaidizi wake wa kazi na kutosababisha mgogoro wowote wa malipo katika eneo la Ujenzi.
13. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kuvunja Mkataba mda wowote atakapo ona inafaa, pale atakapo jiridhisha kuna ukiukwaji wa makubaliano katika Mkataba.
14. **KWAMBA** Endapo kutakuwa na hasara yoyote iliyo sababishwa na mwajiriwa, mwajiriwa atakuwa na wajibu wa kulipa gharama za hasara alizosababisha au kukatwa malipo yake ilikufidia hasara iliyo sababishwa.
15. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshwaji wa kazi uliosababishwa na kucheleweshwa kwa malipo mwajiri atamwongeza muda wa kazi kwa mwajiriwa.
16. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na mwajiriwa mwajiri atakuwa na wajibu wa kuvunja mkataba
17. **KWAMBA** Mwajiri atatoe kusudio la kuvunja Mkataba kwa maandishi ndani ya siku saba.
18. **KWAMBA** mkataba huu ni halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania na utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizi.

HIVYO BASI pande zote mbili zimeweka saini tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonyesha hapa chini:-

KWA AJILI YA USHAHIDI wa makubaliano ya Utekelezaji wa Mkatoba huu,pande mbili zinazohusika wameweka saini zao kama ifuatavyo:

YAMESAINIWA na **KUTOLEWA** na

Saini:.....

Jina: DR. MAGARI MAJURA

Cheo: **MGANGA MFAWIDHI**

Tarehe...10...Mwezi...01...2022



Saini:.....

Jina: Rauli Haseo

Cheo: **MHANDISI WA UJENZI**

Tarehe...10...Mwezi...01...2022

YAMESAINIWA na **KUTOLEWA** na

Saini:.....

Jina: NOAH NDAMBA EDREN

Cheo: **FUNDI KIONGOZI**

Tarehe...10...Mwezi...01...2022

Saini: Rauli

Jina: FESTO A. HAULE

Cheo: **SHAHIDI**

Tarehe...10...Mwezi...02...2022

UKARABATI WA JINGO LA MASHINE YA UPIMAJI WA VIUNGO VYA NDANI YA MWILI WA BINADAMU
(ULTRA SOUND) NA KIPIMO CHA KUANGALIA MOYO (ECG)

NA	AINA YA KAZI	BEI (TSHS)
1	Kubomoa chini, ukuta na sakafu	700,000.00
2	Kuseti njia za umeme	250,000.00
3	Kuseti njia za maji safi na taka	400,000.00
4	Kujenga dari (gypsum)	350,000.00
5	Kupaka rangi	200,000.00
6	Kufunga milango	55,000.00
7	Kufunga umeme	250,000.00
	JUMLA NDOGO	2,205,000.00
8	Kufunga njia za mfumo wa mawasiliano	1,500,000.00
	JUMLA KUU TSH	3,705,000.00

[Handwritten signature]

NBATA NDUMBA EDSON